

MKATABA WA KUUZIANA KIWANJA

Mkataba huu umeingiwa leo tarehe.....¹⁷ Mwezi wa¹⁰ Mwaka 2023

KATI YA

SUSANE KASEGE TIMOTHY wa S.L.P 34651 Kinondoni-DAR ES SALAAM na **TIMOTH M. WILLIAM** wa S.L.P 34651, Kinondoni-DAR ES SALAAM Ambao Katika Mkataba huu wanaitwa "WAUZAJI" kwa upande mmoja ikijumlisha warithi, wakala au mtu yeyote ambaye ana maslahi katika ardhi hii).

NA

GWAJIMA REAL ESTATES CO. LIMITED, wa S.L.P 70777, Dar es Salaam (Ambaye Katika Mkataba huu ataitwa "MNUNUZI) Kwa upande mwingine.

KWAMBA, WAUZAJI ni wamiliki halali wa shamba namba 1678 lililoko Tegeta Salasala wilaya ya Kindoni ndani ya mkoa wa Dar es Salaam lenye hati namba 34544.

KWAMBA, MNUNUZI anataka kununua eneo hilo kwa hiyari yake mwenyewe bila ya ushawishi wa mtu au Taasisi yoyote ile.

HIVYO BASI pande hizi mbili wote wakiwa na akili timamu inakubaliwa ifuatavyo:-

1. Kwamba **WAUZAJI** wanamuuzia **MNUNUZI** eneo la ardhi/shamba tajwa hapo juu kwa bei ya Shilingi za Kitanzania Milioni Mia Nne na Kumi (410,000,000/=) tu.
2. Kwamba **MNUNUZI** amelipa kiasi chote cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa shamba hilo na kwa kusaini mkataba huu, **WAUZAJI** wanakiri kuwa hawana madai yoyote ya ununuzi wa shamba hilo dhidi ya **MNUNUZI**.
3. Kwamba, **WAUZAJI** wataachia umiliki wa ardhi hiyo na kukabidhi nyaraka halisi kwa **MNUNUZI** mara moja baada ya kusaini Mkataba huu.
4. Kwamba, **WAUZAJI** wanakiri kuwa shamba hilo limewekwa rehani katika Benki ya **EQUITY** na kwamba baada ya malipo haya rehani hiyo itaondolewa na shamba hilo litakuwa halina mgogoro wowote na litakuwa mali ya **MNUNUZI**.
5. Kwamba, **MNUNUZI** amekagua na kuridhika na hali ya shamba hilo, na yuko tayari kulinunua kulingana na hali yake.

6. Kwamba, Mnunuzi atakuwa na haki zote za umiliki wa shamba tajwa hapo juu mara tu baada ya kusaini Mkataba huu.

7. Kwamba, Mkataba huu utalindwa na sheria za Tanzania.

KATIKA KUSHUHUDIA HIVYO BASI, Wahusika wanatia saini zao tarehe ya leo kama inavyoonekana hapa chini.

UMESAINIWA na kutolewa hapa DAR ES SALAAM na SUSANE KASEGE TIMOTH ninayememfahamu binafsi leo tarehe 17 Mwezi wa 10 2023

Susane Kasege Timoth

MUUZAJI WA KWANZA


MBELE YANGU:

JINA BENARD SELEMAN MAGUHA

SAHIHI *Maguha*

ANUANI 76932 DAR ES SALAAM

WADHIFA WAKILI



UMESAINIWA na kutolewa hapa DAR ES SALAAM na TIMOTH M. WILLIAM ninayememfahamu binafsi leo tarehe 17 Mwezi wa 10 2023

Timoth M. William

MUUZAJI WA PILI

MBELE YANGU:

JINA BENARD SELEMAN MAGUHA

SAHIHI *Maguha*

ANUANI 76932 DAR ES SALAAM

WADHIFA WAKILI



IMEWEKWA MUHURI WA KAMPUNI YA GWAJIMA REAL ESTATES CO.LIMITED Leo tarehe.....mwezi.....2023

MUHURI WA MNUNUZI

KWA KUSHUHUDIWA NA;

JINA: METHUSELA STIVEN GWAJIMA

SAINI: *Methusela Stiven Gwajima*

ANUANI: 70777

TAREHE: 17/10/2023

WADHIFA: MKURUGENZI

